

TAARIFA HALISI JUU YA KAMPENIYA KUONGEZA KASI YA KUZUIA MAAMBUKIZI YA VIRUSI VYA UKIMWI



(FACT SHEETS FOR THE ACCELERATION OF HIV PREVENTION INITIATIVE)



UTANGULIZI

Taarifa hizi ni tafsiri na hariri za makala zilizotolewa na Shirika la Afya Duniani kuhusu kampeni ya mwaka huu ya kuongeza kasi ya kuzuia maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI katika kanda ya Bara la Afrika. Baadhi ya takwimu halisi nchini Tanzania zimetolewa ili kuleta mlinganisho wa taarifa husika na nchi au sehemu nyingine za dunia hasa Barani Afrika. Kwa kifupi, taarifa zilizotolewa hapa ni muhtasari wa hali halisi katika nchi mbalimbali na hasa katika sehemu za nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara hususani, mashariki, magharibi, kati na kusini mwa Afrika. Ili kupata taarifa hizi kwa usahihi na ufasaha ni vyema msomaji ukazisoma na kuzielewa zote. Taarifa hizi zimetolewa mahsusi ili kama mambo yote yaliyotajwa tukiyazingatia tunaweza kuongeza kasi ya kuzuia maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI nchini na Duniani kwa ujumla.

Vijarida hivi vimesheheni habari muhimu ambazo zimegawanyika katika makundi makuu kumi ya Taarifa kama ifuatavyo:-

1. Kwa nini tuongeze kasi ya kuzuia maambukizi ya VVU ?
2. Kuondoa vikwazo vinavyozuia kujikinga na UKIMWI
3. Tathmini zaidi ni muhimu katika mabadiliko ya tabia
4. Upimaji na Unasihi
5. Uzuiaji wa maambukizi kutoka kwa mama mjamzito kwenda kwa mtoto
6. Uboreshaji wa mfumo wa afya kwa ajili ya huduma bora za Kinga na Tiba ya UKIMWI
7. Tohara kwa wanaume- kupima faida na hasara
8. Watoto na Vijana: Chanzo cha hofu, dirisha la matumaini
9. Wanawake na wasichana: wanaathirika zaidi lakini wanapata huduma duni
10. Vipengele vinne vikuu vinavyochochea kuenea kwa UKIMWI.

Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI

National AIDS Control Programme (NACP),

SLP 11857

Dar es Salaam

Juni 2006